

MASWALI YA KUULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU CHANJO YA COVID-19

Michigan.gov/COVIDvaccine



Je chanjo hii iko salama?

Ndio. Mchakato unaotumiwa kuidhinisha chanjo ya COVID-19 ndio ile ile inayotumiwa kutengeneza chanjo salama na madhubuti za mafua, polio, surua na kifaduro. Ingawa chanjo zinatengenezwa kwa haraka, ni baada ya utafiti wa miaka na majaribio ya kliniki ambayo yamejumuisha watu makumi ya maelfu tofauti waliojitolea kwa hiari. Mchakato wa usalama wa kawaida unabaki kutumiwa na hakuna mkato uliofanyika.